22

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI

NJOMBE URBAN WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY
(MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI NJOMBE)
Website:-www.njuwasa.go.tz
Email:- info@njuwasa.go.tz
S.L.P. 81, NJOMBE,SIMU Na. 0800712323

## MKATABA WA AJIRA YA MUDA MFUPI YA UJENZI WA CHANZO, KUCHIMBA MTARO, KUFUNGA MABOMBA, KUFUKIA MTARO NA UBEBAJI WA VIFAA VYA UJENZI NA MABOMBA.

---

**MKATABA HUU** unafanyika leo tarehe ....15..... mwezi....12......, 20.21.

**BAINA YA**

**MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA NJOMBE (NJUWASA) MKOA WA NJOMBE** (Jina la Mkoa) **S.L.P 81** (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri ") kwa upande mmoja;

**NA**

**JOSHUA JUSTIN MPALALA** (Jina la fundi wa mradi) **S.L.P 24, MAKETE** (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiriwa au fundi Mkuu kwa upande mwingine.

**KWAMBA** kwa pamoja Mwajiri na Mwajiriwa watajulikana kama pande mbili za Mkataba.

**AMBAPO:**

a) Mwajiri ni Taasisi ya Serikali yenye jukumu la kutekeleza ujenzi wa miradi ya maji mjini na kusimamia utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira mjini na yenye makao yake mjini Njombe;

b) Mwajiriwa ni mtu binafsi anayefanya shughuli zake binafsi za ufundi.....MAKETE MJINI.............................................(taja mahali);

c) Mwajiri anakusudia kumwajiri Mwajiriwa kwa kipindi cha muda mfupi wa siku ...TISINI (90)..............

Mwajiriwa anakubali matakwa ya Mwajiri na anakubali kwa hiari yake mwenyewe kuajiriwa kwa muda mfupi kama **Fundi Mkuu kwenye ujenzi wa chanzo isapulano, ubebaji wa vifaa vya ujenzi kutoka kijijini isapulano hadi eneo la ujenzi, uchimbaji wa mtaro na kufunga mabomba kwa umbali wa Km 4.9**

d) **MKATABA HUU UNASHUHUDIA** kwa pande zote mbili kukubaliana kama ifuatavyo:

## 1. MADHUMUNI YA MKATABA

Mkataba huu ni kwa ajili ya **kufanya ujenzi wa chanzo isapulano, kufunga mabomba na ubebaji wa vifaa vya ujenzi** ambapo Mwajiriwa atapaswa kufanya kazi zifuatazo kama zinavyosomeka na gharama zake:

a) Kusafisha eneo la ujenzi (site clearance) $15M^2$ @80,000 Tsh 1,200,000/

b) Kusawazisha eneo la ujenzi $15M^2$ @105,000 Tsh 1,575,000/

c) Uchimbaji wa msingi na ujenzi wa msingi $8M^3$ @ 250,000 Tsh 2,000,000/

d) Ujenzi wa kuta za intake na kufanya finishing ya intake $15M^3$ @220,000 Tsh 3,300,000/

e) Kuunganisha bomba na kufunga fittings kwenye intake itakayojengwa kulingana na mchoro 4pcs @145,000 Tsh 580,000/

f) Kusogeza vifaa vya ujenzi eneo la ujenzi wa intake kokoto, mchanga, mawe, cement, nondo kulingana vifaa tajwa kwenye BoQ Tsh 3,500,000/

g) Uchimbaji wa mtaro 4,900 na ufukiaji kwa kipimo cha kina 1mx40 wide. 4900M @1200 Tsh 5,880,000/

h) Ubebaji wa bomba za 225mm na kuzisogeza na kupanga sambamba na mtaro Tsh 850,000/

i) Kuunga bomba za PVC 250 na 225mm umbali wa mita 4900M @400 Tsh 1,960,000/

j) Ujenzi wa valve chamber na air valve 3 @50,000 Tsh 150,000/

k) Kuunganisha maji kwenye tanki Kijiji cha Isapulano Tsh 450,000/

**JUMLA TSH 21,445,000/=**

## 2 MUDA WA UTEKELEZAJI WA KAZI

Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku TISINI (90), ambapo itaanza tarehe 15.12.2021 na itakamilika tarehe 17.03.2022.

**MALIPO YA UTEKELEZAJI WA KAZI ULIOKUBALIA KWA PANDE ZOTE MBILI**

a) Mwajiriwa atalipwa jumla ya kiasi cha Tshs. 21,445,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hii na utaratibu uliokubalika kwa pande zote mbili ni kama ifuatavyo;

   i. Ujenzi wa Intake malipo yataanza kufanyika baada ya kazi kufikia asilimia 30 na kuendelea

   ii. Uchimbaji wa mtaro na ufungaji wa bomba malipo yataanza kufanyika baada ya kazi kufikia asilimia 30 na kuendelea

   ***MUHIMU***

   ***Hii itafanyika baada ya timu ya ukaguzi kukagua kazi na kufanya tathimini ya kazi iliyofanyika kufikia kiwango cha asilimia 30 na kuendelea.***

b) Malipo ya Mwajiriwa yatakuwa ni kwa fedha za kitanzania tu (*Tanzanian Shillings*);

c) Malipo hayo yatalipwa kwa hundi ambayo yatalipwa benki;

d) Malipo ya Mwajiriwa yatalipwa kwa awamu awamu kulingana na kazi iliyofanyika kwa tathimini ya asilimia 30 na kuendelea.

e) Kabla ya malipo ya mwisho kufanyika,Mwajiriwa anapaswa kuwasilisha taarifa zote zinazohitajika na kufanya marejesho ya vifaa vyote vya kazi iwapo atakuwanavyo.

## 2. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRI

Mwajiri ambaye atawakilishwa na Msimamizi wa Kazi, atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

a) Kusimamia na kuthibitisha ubora wa kazi inayofanywa na fundi.

b) Endapo kazi itakayofanywa na Mwajiriwa haitafikia viwango vya ubora unaotakiwa, Mwajiri atachukuwa hatua stahiki dhidi ya Mwajiriwa huyo; na Msimamizi wa Mradi ata mtaarifu fundi wa kazi hii kwamba ameshindwa kutimiza masharti ya makubaliano.

c) Kuhakikisha kuwa endapo Mwajiriwa atafanya kazi isiyokidhi viwango au isiyoridhisha, Mwajiriwa huyo anarekebisha au kurudiwa upya kazi hiyo kwa gharama zake mwenyewe.

## 3. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRIWA

Mwajiriwa ambaye ni Fundi ujenzi atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

a) Kuhakikisha kuwa anatekeleza majukumu yake kama ilivyoelekezwa kwenye sehemu ya 1 (Madhumuni ya Mkataba) kulingana na ramani na vipimo viliyotolewa na Mwajiri;

b) Kuhakikisha kuwa anawajibika kufanya kila jambo ambalo kwa ujumla wake litaleta mafanikio kwenye kazi;

c) Atatekeleza majukumu yake kwa uaminifu, uadilifu, umakini na weledi mkubwa na endapo atatekeleza kinyume na matakwa haya, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake;

d) Atawajibika kwa Msimamizi wa Mradi (*Project Manager*) kwa utendaji wake wa kila siku na atatekeleza maelekezo anayopewa na kiongozi huyo;

e) Atawajibika kuhudhuria mikutano ya tathmini ya mradi pamoja na watendaji wengine wa timu yake kila itakapopangwa;

f) Atawajibika kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mradi kila zitakapohitajika;

g) Kuhakikisha malipo ya vibarua na mafundi walioajiriwa kwa mikataba midogo yanafanyika kwa wakati; na

h) Kufanya usafi eneo la ujenzi wa mradi na kuondoa mabaki yote ya vifaa vya ujenzi na kuviweka katika eneo litakaloelekezwa na Msimamizi wa Mradi.

**4. HAKI NA WAJIBU WA WANANCHI WA SEHEMU HUSIKA YA UJENZI WA MRADI WA MAJI/WANANCHI**

Wananchi watakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

a) Kushiriki katika vibarua vya kazi ndogo ndogo za kulipwa kwaajili ya kushirikiana na mafundi;

b) Kutekeleza majukumu mengine pale inapohitajika kwa maelekezo ya Msimamizi wa Mradi.

**5. UTOAJI WA MIKATABA MIDOGO**

Mwajiriwa anaweza kuingia Mikataba midogo kiasi kadhaa ya utekelezaji wa kazi na vibarua (*casual labourers*) watakaokuwa chini ya usimamizi wake.

**6. UCHELEWESHAJI WA UTEKELEZAJI WA MRADI**

Endapo kazi haitakamilika katika muda uliopangwa, Mwajiriwa atalipa faini ya asilimia 0.01%... (weka asilimia) ya malipo ya kazi yote kwa kila siku ya ucheleweshwaji isipokuwa kukiwa na sababu ya msingi ya ucheleweshwaji wa kazi ulioidhinishwa kwa maandishi na Msimamizi wa Mradi.

**7. DHAMANA YA UHARIBIFU**

a) Mwajiriwa atawajibika kulipa gharama za uharibifu au madhara yoyote yatakayosababishwa na wafanyakazi wake au vifaa vyake wakati wa utekelezaji wa mradi; na

b) Gharama hizo au madhara hayo yatabainishwa na Msimamizi wa Mradi kwa maandishi.

## 8. SHERIA ITAKAYOTUMIKA

Mkataba huu utaongozwa na kusimamiwa na Sheria za Tanzania.

## 9. USULUHISHI WA MGOGORO

Endapo kutatokea mgogoro wa aina yoyote baina ya Mwajiri na Mwajiriwa kuhusu utekelezaji wa mradi huu:

a) Pande zote mbili zitatatua mgogoro huo kwa njia ya amani ya mazungumzo ambapo makubaliano ya pande hizi mbili yatapelekea Mkataba huu kufanyiwa marekebisho; na

b) Endapo mgogoro huo utashindikana kutatatuliwa kwa njia ya amani ya mazungumzo, pande zote mbili zinaweza kuchukua hatua stahiki za kisheria kwa mujibu wa Sheria za Tanzania.

## 10. KUSITISHA MKATABA

Mkataba huu unaweza kusitishwa endapo upande mmoja au pande zote mbili za Mkataba zitashindwa kutekeleza wajibu wake au masharti ya Mkataba huu.

## 11. MAREKEBISHO YA MKATABA HUU

Kwamba Mwajiri na Mwajiriwa wanaweza kubadilisha baadhi ya masharti ya Mkataba huu kwa makubaliano ya pamoja kwa njia ya maandishi.

**KWA USHUHUDA HUU**, pande zote mbili zinaweka saini zao katika Mkataba huu siku na tarehe kama ilivyooneshwa hapa chini:

---

**KWANIABA YA MWAJIRI (NJUWASA)**

**Jina:** Eng John F. Kifyaudi

**Saini:** [signature]

**Cheo:** MKURUGENZI MTENDAJI

**Tarehe:** 15/12/[illegible]

Stamp: MBE WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY (NJUWASA) P.O. BOX 81 NJOMBE

**Shahidi:**

**Jina:** ENG YONAS NDOMBA

**Saini:** [signature]

**Cheo:** MD MAKETE

**Tarehe:** 15/12/2021

Stamp: MAKETE WATER SUPPLY AUTHORITY MAKEWASA P. O. BOX 54 - MAKETE.

---

**KWANIABA YA MWAJIRIWA (FUNDI)**

**Jina:** JOSHUA JUSTIN MPALALA

**Saini:** [signature]

**Cheo:** FUNDI MKUU

**Tarehe:** 15.12.2021

**Shahidi:**

**Jina:** Martha L. Kitta

**Saini:** [signature]

**Cheo:** fundi msaidizi

**Tarehe:** 15. 12. 2021.

---

## SEHEMU II: MCHANGANUO WA GHARAMA ZA UFUNDI
## MCHANGANUO WA GHARAMA ZA UFUNDI MRADI WA ISAPULANO-MAKETE

| S/N | Item Code | MAELEZO | KIPIMO | IDADI | BEI | JUMLA (Tshs.) | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| *(1)* | *(2)* | *(3)* | *(4)* | *(5)* | *(6)* | *(7)* | |
| | | **NJIA KUU YA MAJI** | | | | | |
| 1 | | **UJENZI WA INTAKE.** | | | | | |
| | a | **Kusafisha eneo la ujenzi(site clearance)** | $M^2$ | 15 | 80,000 | 1,200,000/= | |
| | b | **Kusawazisha eneo la ujenzi** | $M^2$ | 15 | 105,000 | 1,575,000/= | |
| | c | **Uchimbaji wa msingi na ujenzi wa msingi** | $M^3$ | 8 | 250,000 | 2,000,000/= | |
| | d | **Ujenzi wa kuta za intake na kufanya finishing ya intake** | $M^3$ | 15 | 220,000 | 3,300,000/= | |
| | e | **Kuunganisha bomba na kufunga fitting kwenye intake itakayojengwa kulingana na mchoro** | Pcs | 4 | 145,000 | 580,000/= | |
| | | **SUB TOTAL (i)** | | | | 8,655,000/= | |
| 2 | | **UJENZI WA GRAVITY MAIN** | | | | | |
| | a | **Kusogeza vifa vya ujenzi eneo la ujenzi wa intake. Kokoto, mchanga mawe,cement,nondo. Kulingana na vifaa tajwa kwenye BoQ** | Lump sum | 1 | 3,500,000 | 3,500,000/= | |
| | b | **Uchimbaji wa mtaro 4,900 na ufukiajia.kwa kipimo cha kina1mx40 wide** | M | 4,900 | 1200 | 5,880,000/= | |
| | c | **Ubebaji wa bomba za 225mm na kuzisogeza na kupanga sambamba na mtaro** | Lump sum | 1 | 850,000 | 850,000/= | |
| | d | **Kuunganisha bomba za PVC 225mm umbali wa mita 4,900 M** | M | 4,900 | 400 | 1,960,000/= | |
| | e | **Ujenzi wa valve chamber na airvalve** | Ea | 3 | 50,000 | 150,000/= | |
| | f | **Kuunganisha maji kwenye tank** | Lump sum | 1 | 450,000 | 450,000/= | |
| | | **SUB TOTAL (ii)** | | | | 12,790,000/= | |
| | | **TOTAL COST CONSTRUCTION WORKS** | | | | 21,445,000/= | |

*JINA LA FUNDI*: JOSHUA JUSTIN MPALALA

*ANUANI YAKE*: S.L.P. 24. MAKETE.

**KUMBUKUMBU ZA KIKAO CHA MAJADILIANO KATI YA JOSHUA JUSTINE MPALALA NA TIMU YA MAJADILIANO KOTESHENI YA FUNDI UJENZI TAREHE 08/12/2021**

**WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Majuto Komba | Mwenyekiti |
| 2. | Hery Kyando | Katibu |
| 3. | Nyitike Ngulwa | Mjumbe |

**AGENDA No. 1: MUHT. Na.01/Neg/01/2021/2022 KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua Kikao saa 10:30 Asubuhi kwa kuwakaribisha Wajumbe kushiriki Kikao.

Mwenyekiti aliomba ushirikiano wa hali na mali ili zoezi liweze kufanikiwa na ili kuipata thamani ya hela (Value for Money)

**AGENDA No.2: MUHT.Na.01/Neg/01/2021/2022 KUPOKEA AGENDA ZA KIKAO**

Timu ya negatiation ilipokea agenda tano (4) za kikao bila mabadiliko yoyote kwa ajili ya kujadiliwa kama ifuatavyo:

1 Kufungua Kikao.
2 Kupokea Agenda.
3 Kujadili punguzo la gharama za ujenzi wa intake, ubebaji vifaa vya ujenzi na kuchimba mtaro, kufunga bomba na kufukia mtaro.
4 Kufunga Kikao.

**AGENDA No. 3: MUHT. Na.01/Neg/01/2021/2022 OMBI LA KUPUNGUZIWA GHARAMA YA UJENZI WA INTAKE, UBEBAJI VIFAA VYA UJENZI NA UCHIMBAJI MTARO KUFUNGA BOMBA NA KUFUKIA MTARO MITA 4900**

Baada ya mjadala mrefu kufanyika fundi aliweza kupunguza kiasi cha Tsh **505,000/=** ambapo gharama ilishuka kutoka **21,950,000/=** hadi **21,445,000/=**

Kazi itakamilika ndani ya miezi mitatu (3) kwa ufanisi na ubora uliokusudiwa baada ya kusaini Mkataba.

**AGENDA No. 4: MUHT. Na.01/Neg/01/2021/2022 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 11:10 asubuhi kwa kuwashukuru wajumbe wote kwa ushirikiano waliouonyesha katika kujadili agenda za kikao.

| | |
|---|---|
| ................................ | ................................ |
| **Katibu** | **Mwenyekiti** |
| **Tarehe** 08/12/2021 | **Tarehe** 08/12/2021 |